

# BATA WA MUSCOVY

NA F. BAUER,  
POULTRY RESEARCH CENTRE, LABU, PAPUA NEW GUINEA  
Chapisho 1983

*Tafsiri na:* PATRICK BUNYALI KAMOYANI Agosti 2005

---

## MAKALA YA ECHO

---

### MAELEZO

Bata wa aina ya Muscovy ni ndege mkubwa, hufa sana kwa ajili ya nyama. Kwa utunzaji bora, na lishe lifaalo, aina ya bata wakubwa (wale wa kiume) hufikia uzani wa 4.0-4.5kg huku wale wa kike wakifikia uzani wa 2.0-2.5kg baada ya wiki 16, huu ndio umri wa kuuza au kuchinja bata. Idadi kubwa ya bata wa Muscovy ni wa rangi nyeupe hata hivyo kuna aina ya rangi nyeusi. Kuna idadi nyingine kubwa iliyo na weupe na weusi. Ndege hawa huwa na nyama nyekundu kwenye sehemu ya macho na mdomo. Miongoni mwa bata wa kiume, rangi hiyo huonekana mgongoni na kwenye shingo na mabawa. Iwapo bata watapata lishe bora, basi unaweza kutarajia mayai 90 kwa mwaka na kuangua vifaranga pasipo matatizo. Jamii hii ya bata yaweza kuwachiliwa huru ili kujitafutia lishe. Kama ilivyo kawaida kule Papua New Guinea (PNG) wakulima hawajali sana jinsi ya kuwalisha bata na hutegemea tu mbinu hai za uzalishaji. Bata huyu wa Muscovy amefaulu sana katika vijiji vya PNG.

### KUTUNZA BATA

#### KUTOKA 0 HADI WIKI 6

##### *Eneo la mradi*

Katika kilimo cha kufuga bata, chagua eneo: (1) karibu na kijiji, ili kuwatunza kwa urahisi, (2) mahali palipo na kivuli (usiwaache bata kwenye jua kwa muda mrefu), (3) mahali palipo na nyasi au kwekwe ili bata watonogoe na kutafuta wadudu, (4) eneo lisilo karibu na ua la nguruwe (kwa mara nyingi, nguruwe hua na kula bata), (5) mahali pasipo na mwewe wengi, (6) karibu na kidimbwi, panapo uwezekano. Epuka sehemu kavu, zilizo na jua kali, au funika kwa nyasi za kunai.

##### *Vyumba*

Chumba kidogo cha 3 x 5m, kilichojengwa kwa viungo vinavyopatikana kwa urahisi hutosha kuweka bata 20. Hakikisha kwamba kuna mwangaza wa kutosha ili bata waweze kukua kwa urahisi. Hali kadhalika hakikisha kwamba chumba hicho hakitafikiwa na mbwa na paka. Gawa na kutenga eneo ndogo ndani ya chumba hicho (kiasi cha .5 x .5 x .3 m) mahali ambapo bata watalala na kuingia wakati wa baridi. Weka matandiko kwenye sakafu. Matandiko yaweza kuwa machujo ya mbao, ubua, machujo ya kahawa, au aina ya viungo vikavu vya kunai. Matandiko haya hayapaswi kupata unyevu.

---

ECHO, 17391 Durrance Rd., North Ft. Myers FL 33917, USA.

SIMU- (941) 543-3246; Kipepesi: (941) 543-5317

Barua-pepe- [echo@echonet.org](mailto:echo@echonet.org); Mtandao- <http://www.echonet.org/>

### *Lishe na Maji*

Licha ya kuwa ghali, ni bora kuwapatia bata vyakula bora vilivyoimarishwa kwa muda wa wiki za kwanza sita. Aina ya chakula cha mwanzo (*Broiler starter*), (*pullet starter*), (*broiler finisher*) ndio hufa. Usitumie aina ya chakula cha kutaga mayai kwani aina ya vyakula kama hivi hukosa protini. Kifaranga wa bata atatumia 3 kg za chakula kwa muda huu. Baada ya wiki tano, waweza kutafuta aina ya vyakula vingine vinavyopatikana kwa urahisi kwa pamoja na lishe lililo tayarishwa. Kila aina ya chakula cha binadamu hufa bata. Aina ya mmea wa Choko, majani na matunda yake ni chakula kizuri sana kwa bata.

Usiweke zaidi ya vifaranga 40 mahali pamoja. Idadi kubwa ya vifaranga huhitaji chakula kingi, jambo ambalo laweza kuwa tatizo kwa mkulima, na pia kuathiri ukuaji. Iwapo bata wataangua zaidi ya vifaranga 40 kwa wakati mmoja, itakuwa bora kuuza au kugawa kwa wakulima wenzako wale wa ziada.

Maji yapaswa kuwepo kila mara. Waweza kutengeneza vifaa vya maji kutoka kwa mwanzu. Hali kadhalika ni vyema kuwepo na kidimbwi mahali pa bata kunywa na kucheza ndani ya maji, hata hivyo sio lazima. Pipa la lita 200 (44-gallon) lililokatwa, au sufuria kubwa hufa sana, huku ukiongeza maji yanapopungua au kuchafuliwa sana.

### *Kutunza vifaranga*

Ni vyema kutenganisha vifaranga na bata wakubwa, kwani huenda waka shambuliwa na hata kuuawa. Chukua vifaranga baada ya kuanguliwa unapohakikisha kwamba wako imara na kisha kuweka kwenye sehemu ya kuwatunza vyema kama ilivyoielezwa hapo juu. Waweza kujenga chumba kipya cha vifaranga au kutumia chumba cha hapo awali.

Katika sehemu za pwani, hadi mwinuko wa 1000m, vifaranga wa bata wanaweza kujitunza wenyewe. Wiki za kwanza tano, vifaranga wapaswa kuwa ndani ya chumba kwa wakati wote. Katika wiki ya sita waweza kuwafungulia, kwa muda wa saa chache kila siku. Itakuwa ni vyema kwa mtu kuwatunza kwa muda huo. Katika maeneo ya nyanda za juu (mwinuko wa 1000m), hali ya ubaridi yaweza kuwa shida wiki za kwanza mbili. Yafuatayo ni maelezo kuhusu jinsi unavyoweza kukabili matatizo kama hayo: (1) Weka vifaranga katika mahali palipo na ukavu katikati ya chumba kwa wiki mbili. (2) Tengeneza eneo ndogo la mduara kuzunguka, mduara wa mita moja kwa kutumia mabati, kapu lililo fumwa kwa kutumia mianzi, mbao nyepesi, n.k, kisha kufunika, na kuwacha eneo moja wazi, upana wa 30cm katikati. Weka taa ndani ya eneo hilo, kwenye lile eneo lililo wazi. (3) Chukua sanduku la karatasi (kama lile la bidhaa) na kutoboa mashimo. Kila usiku au hali ya anga inapobadilika, weka vifaranga kwenye sanduku hilo na kufunika. Wachilia vifaranga asubuhi, au hali ya anga inapoimarika. Wakati wa mchana usiweke vifaranga kwa sanduku hilo kwa zaidi ya saa mbili. (Kisanduku cha bidhaa kama bia chaweza kutosheleza vifaranga 10.)

### **KUTOKA WIKI 6 HADI MIEZI 4**

Baada ya wiki sita, bata waweza kupewa vyakula vya kawaida vinavyopatikana kwa urahisi--viazi vitamu, taro, ndizi, malenge, choko, n.k. Aina ya chakula kifaacho binadamu pia chaweza kutumiwa kama lishe. Chakula hicho chapaswa kupikwa. Ili kuelewa viwango vya lishe kwa bata, tumia utaratibu huu: Iwapo bata watakula kila kitu pasipo kubakisha kwa muda wa nusu saa, basi hawajashiba. Wakati mwingine ongeza kipimo. Iwapo baada ya nusu saa, bata wameacha chakula, basi wametoshika.

Lishe la bata kwa kutumia viungo vilivyoko kwa urahisi haitoshelezi tu. Kila siku bata wafaa kutembea na kutonogoa nyasi au kwekwe. Ni kwa kutembea wakichakura wadudu na kutonogoa mimea ndiposa watapata protini ya kujenga miili. Protini hii itatoka kwa wadudu na mbegu za kwekwe au nyasi. Hata sehemu kubwa iliyozungukwa na ua haiwezi kutoa nafasi ya kutosha kwa lishe, kwa sababu bata watamaliza nyasi katika eneo hilo. Hatupaswi kuwepo ua katika eneo hilo.

Mradi ulio zungukwa na ua hauwezi kufaulu. Ni bora kupoteza idadi ndogo ya bata kwa mahasimu kama mbwa kuliko kupoteza idadi yote kwa kukosa lishe bora. Ukosefu wa protini waweza kusababisha: (1) Ukuaji duni--bata haitaweza kufikia uzani unaofaa, (2) kukosa mabawa--baridi yaweza kuwa nyingi, kuleta magonjwa na hatimaye kuangamia, (3) Kukosa kutaga mayai--bata hawataweza kutaga mayai.

Njia bora ya kutunza bata baada ya wiki sita ni kuwaweka ndani ya nyumba usiku na kuwa achilia saa mbili asubuhi. Wakati huo wanahisi njaa na watakuwa na bidi ya kutafuta wadudu na nyasi. Kabla ya kuingia usiku hakikisha bata wamepata lishe la kutosha. Itakuwa vyema iwapo utatumia aina moja ya mlio kuwaita bata (kwa mdomo, kengele, n.k.). Watakuja kwa haraka pasipo kuwaelekeza. Fungia bata usiku. Weka maji kwenye chumba chao.

Baada ya miezi minne, bata watakuwa wamefikia uzani kamili. Katika mandhari ya vijiji, uzani wake utakuwa 2.0kg wale wa kiume na 1.2kg kwa wale wa kike. Ni wakati wa kuchinja au kuuza, la sivyo nyama yake itakuwa ngumu. Usiweke bata mdogo baada ya muda huo ukitumai kwamba ataongeza uzani. Itakuwa ni kupoteza muda na lishe

### KUZALISHA BATA

Ni rahisi sana kwa mkulima kuzalisha bata kuliko kununua nje, mkulima apaswa kuendeleza ufugaji huu mwenyewe. Dumisha bata walio na afya bora kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji. Kwa kuzingatia haya, vifaranga watakuwa na nguvu na afya bora. Usiweke ndege waliolemaa au wenye umbo lisilo la kawaida kwa ajili ya uzalishaji. Usipozingatia hayo utapata ndege wengi wasio na umbo la kawaida. Usiweke aina ya ndege wenye umbo ndogo. Ndege wakubwa na wanene huzalisha kizazi kilicho na sifa hizo. Ndege walio nuiwa kwa shughuli hii wapaswa kuwa wanene kiasi kwamba tumbo inashika chini. Bata wa kiume wapaswa kuwa na umbo nene. Usiweke bata aliyechukua umbo mfano wa kusimama imara. Usiweke zaidi ya bata 10 kwa ajili ya uzalishaji. La sivyo lishe halitaweza kuwatosheleza bata wengi. Fuga bata wa kiume wawili kwa kila bata watano na watatu kwa bata kumi. Bata waweza kufugwa kwa hadi miaka mitatu, lakini wale wa kiume wapaswa kubadilishwa baada ya miaka miwili, kwani huo ndio umri ambao nguvu zao hudidimia na kukosa uwezo wa kuzalisha.

#### *Kutaga mayai*

Katika mandhari ya kijiji, bata huanza kutaga mayai wanapofikia miezi 8 1/2 - 9. Mayai ya mwanzoni yatakuwa madogo na hayapaswi kutumiwa kwa kuangua vifaranga. Mayai madogo kwa kawaida hayatakuwa na uwezo wa kuangua (vifaranga hawataibuka) na hata iwapo yataanguliwa, vifaranga watakuwa wadogo na wasio na afya nzuri na kufariki katika wiki ya kwanza. Yai huwa na uwezo wa kuanguliwa endapo uzani wake ni gramu zaidi ya 72g au iwapo mduara wake ni zaidi ya 45mm. Njia bora ya kupima uwezo wa yai kuangua ni kutengeneza shimo kwenye mbao nyepesi, shimo la mduara wa 45mm. Iwapo yai litapita kwenye shimo hilo, basi ni ndogo sana na lapaswa kupikwa au kuuzwa. Iwapo yai haliwezi kupita kwenye shimo hilo, basi weka kwa ajili ya uzalishaji. Kituo cha utafiti kuhusu ufugaji kule Labu kimeonyesha aina ya mashimo hayo.

Bata atataga mayai kati ya 10 na 20. Kisha baadaye atataka kuyakalia mayai yale. Iwapo bata atanyang'anywa vifaranga, basi huanza kutaga mayai baada ya muda mfupi miezi miwili hadi minne, kulingana na aina ya lishe. Hakuna msimu wa kutaga mayai kule Papua New Guinea. Bata hutaga mayai mwaka mzima.

Iwapo itagunduliwa kwamba, katika mradi, bata hawatagi mayai baada ya miezi 12, kuna shida. Labda bata hawapati lishe la kutosha na kukosa protini kwa viwango vifaavyo. Bata walio pitisha umri huo bila kutaga mayai wapaswa kuchinjwa au kuuzwa na mradi kusimamishwa. Hata hivyo, imeweza kushuhudiwa kwamba bata wenye afya (wenye mabawa kamili, uani unaozidi 1.3 kg)

hukosa kutaga mayai kwa sababu zisizoeleweka. Iwapo haya yataokea, hamisha mradi hadi eneo lingine, eneo lililo na mimea tofauti. Iwapo hakuna tofauti katika kipindi cha miezi sita, simamisha mradi huo. Katika miradi mingi bata hukosa kutaga mayai. Bata kama hao wapaswa kuchinjwa au kuuzwa. Bata asiyeweza kutaga mayai hutambuliwa kwa tabia zifuatazo: (1) ni mzito kuliko wengine, (2) nyama iliyo kando ya macho ni nyekundu sana, kama bata wa kiume badala ya rangi ya machungwa au ekundu-nyeupe, (3) nafasi kati ya mifupa miwili ya upande wa chini (inayoelekeza sehemu ya kutaga mayai) ni upana wa kidole kimoja badala ya 2 au 3.

#### *Viota*

Viota vyapaswa kujengwa ili bata waweze kutaga mayai kwenye viota hivyo. Idadi ya viota yapaswa kuwa sawa na ile ya bata. La sivyo watasumbuana kwa kujitafutia viota au kukalia kiota kimoja bata wawili, jambo lisilo bora. Bata wawili kwenye kiota kimoja hawawezi kuangua vifaranga wengi ukilinganisha na bata mmoja kwenye kiota.

Viota vyapaswa kuwa 30 x 30 x 40 cm (12 x 12 x 16") na kufunikwa. Hii ni kuzuia bata wawili wasikalie kiota kimoja na pia wale wa kiume wasiende kwenye kiota. Weka mbao, upana wa 5cm (2") upande wa mbele, ili mayai yasiweze kusonga na pia ni bora kuweka matandiko kama vile machujo ya mbao, machujo ya kahawa, n.k. Dumisha usafi kwenye kiota kila mara.

#### *Umuhimu wa Bata wa Kiume*

Inaaminika kote kule Papua New Guinea kwamba ndege wa kiume ni muhimu kwa ndege wa kike (kuku, bata, bata mzinga, n.k.) ili kutaga mayai. Dhana hii sio kweli. Ndege wa kike ataendelea tu kutaga mayai bora tu kuna lishe bora na la kutosha na hakuna shida ya magonjwa. Iwapo ndege wa kiume (jogoo, bata wa kiume, *tom turkey*, n.k.) atakuwepo, ndege hao wataweza kupata mayai yaliyo na uwezo wa kuangua vifaranga. Iwapo hakuna ndege wa kiume basi mayai hayataweza kuangua vifaranga, yataharibika, na hayataweza kuanguliwa hata iwapo bata wa kike atakalia. Iwapo bata hatagi mayai, usije ukalaumu bata wa kiume, ila tu imarisha lishe au chunguza iwapo kuna maradhi.

#### *Kutunza Mayai*

Itikadi nyingine ya kupotosha ni kwamba mayai yakishikwa na watu hayawezi kuanguliwa. Mayai yaweza kuokotwa na kuhifadhiwa kwenye nyumba kwa siku saba. Mayai hayo huangua endapo yatakaliwa. mayai yaliyo kaliwa yaweza pia kuguswa, lakini ya rudishwe mara moja. Mayai ambayo yatapoteza joto lake kwa muda mrefu huharibika. Hata hivyo, iwapo mayai yatateleza kutoka kwa viota wakati wa usiku, itafaa kurudisha kwenye kiota kwani hayajaharibika. Hii ni kweli hasa sehemu za pwani.

#### *Kuangua*

Bata wa Muscovy hukalia mayai kwa wiki tano (siku 35-37) kabla ya vifaranga kuanguliwa. Itachukua kati ya saa 12 na 24 kati ya kupasuka kwa yai hadi kuondoka kwa kifaranga. Usijaribu kwa wakati wowote kuwasaidia vifaranga kutoka kwa yai. Ila tu iwapo kichwa cha kifaranga kiko nje huku sehemu nyingine ya mwili ikisalia kwenye yai au iwapo ganda la yai limeonyesha ishara ya kupasuka na kifaranga hakijatokeza kwa kikamilifu.

Usipanue yai unapoono ganda limeanza kupasuliwa. Kwa kawaida mayai yote yapaswa kuanguliwa baada ya siku mbili (kwani vifaranga huanza kukua punde tu mayai yanapokaliwa). Iwapo baada ya siku hizi mbili, mayai yatakuwa hayajaanguliwa, basi kagua. Iwapo mayai yanaonekana ya rangi ya samawati au kuna vidota vya samawati, au unapotingisha ni kama kuna maji, yai hilo ni bovu na lapaswa kutupwa.

Iwapo yai linang'aa na ni la rangi nyeupe, na kudumisha joto hata baada ya kutokaliwa kwa muda, yai hilo ni nzuri. Ni bora kuliweka kwenye kiota kingine kilicho kaliwa. Iwapo hakuna, bata apaswa

kuendelea kukalia, lakini sio kwa zaidi ya wiki mbili, iwapo utapitisha muda huo, bata hupoteza uzani na hata kufa. Iwapo hakuna mayai kwenye kiota, safisha na kubadilisha matandiko.

**Majulisho:**

Makala haya yametafsiriwa na;  
Patrick Bunyali Kamoyani  
P.O Box 1, 50321-Magada via Maragoli, Kenya  
Simu: +254 (0) 721 612 607

Barua-pepe: [pbkamoyani@excite.com](mailto:pbkamoyani@excite.com) au [pbkamoyani@lycos.co.uk](mailto:pbkamoyani@lycos.co.uk)